# Ushirikishwaji Wa Kila Mshiriki

HUDUMA BINAFSI
MPANGOKAZI WA IDARA

2017 – 2020

Shule ya Sabato GC na
Idara ya Huduma Binafsi




Kanisa lisilotumia huu mtindo wa uinjilisti, haliwezi kukua wala washiriki wake hawezi kukomaa kioroho.......

Adopted From GC
By Pr. Almodad Amos

# Kuhamasisha kila Mshiriki
## kwa ajili ya utume
## Kupitia Idara ya Huduma Binafsi

REACH the WORLD

STRATEGIC PLAN 2015–2020

**Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi. (Matendo 1:8)**

# Idara ya Huduma Binafsi
## *Mpango Kazi*

Ukweli unapaswa kusambazwa na wote wanaokiri kuwa wanafunzi

—*Christian Service, p. 68.*

## Ushirikishwaji wa Kila Mshiriki

Utume Wetu: Utume wa Idara ya Huduma Binafsi ni kutoa miongozo na mafunzo kwa kusudi la kumuhusisha kila Mwadventista Msabato katika huduma ya uongoaji wa roho. Suala la kuwafundisha na kuwahusisha washiriki wote kanisani ni jambo la msingi sana kwetu ikiwa tunakusudia kuimaliza kazi tuliyopewa. Hili ni jambo la msingi sana kwa kuwaandaa washiriki kiroho na kwa mafanikio ya uinjilisti wa nje, tukiwa na injili ya milele ya ujumbe wa malaika watatu.



Goli Letu: *Kufanya Wanafunzi!*

HUDUMA BINAFSI

MPANGOKAZI

2017 – 2020

Shule ya Sabato na Huduma Binafsi

## KUMFIKIA MUNGU Ili kufanya wanafunzi, lazima kwanza tufanyike wanafunzi.

KUSUDI: Kumuongoza kila mshiriki kumkaribia Mungu kwa kupitia maombi binafsi, Kujifunza Biblia nyumbani, na kuwa na Ushirika pamoja na Yesu katika maisha ya kila siku. Kama Kanisa halijawafikisha hapa washiriki, uinjilisti hautafanikiwa katika Kanisa hilo.

### Jinsi ya Kumfikia Mungu kupitia Huduma binafsi

Ili kuwahudumia wengine kwa upendo katika huduma hii ya uongoaji wa roho, tunpaswa kuwaelekeza washiriki jinsi ya kufanya maombi binafsi. Ili tuwe tayari kwa ajili ya kuipeleka injili, tunapaswa kuwa na muda mzuri sana wa kuwafundisha washiriki jinsi ya kuisoma na Kujifunza Biblia wakiwa wenyewe. Hatimaye sasa tunaweza kuwafundisha jinsi ya kufanya program ya uongoaji wa roho. Kiongozi apange muda maalum wa kuwafundisha na kuwaelekeza washiriki kwa umakini jinsi ya kuisoma Biblia kwa namna rahisi na kufanya maombi. Ktk maombi hayo, waelekeze kumuomba Mungu kuwasaidia kuwa na moyo wa kimeshenari, kuelewa jinsi ya kufanya uinjilisti na wamuombe Mungu awasaidie kujiunga na idara mbalimbali ndani ya Kanisa.



**Kipimo**

- *Washiriki waongozwe katika kufanya uamsho na matengenezo kupitia maombi binafsi na Kujifunza Biblia*
- *Kuona mahudhurio yakiongezeka katika Shule ya Sabato, katika Ibada Kanisani na Ibada za Maombi.*
- *Ongezeko la washiriki kujiunga na kushirikishwa katika program za Idara mbalimbali na ushiriki wao katika kushuhudia.*

## KUWAFIKIA WENZETU Yesu hakutuamuru kufanya washiriki, bali wanafunzi (Tazama Mathayo 28:19)

KUSUDI: Kuwaongoza washiriki kuwa wanafunzi kwa namna endelevu ya kuwalea, kuwafundisha {Jinsi ya kuwa na kufanya wanafunzi}, na kuwakomaza katika imani kwa kuwaelekeza.

### Jinsi ya Kuwafikia Wenzetu kupitia Idara ya Huduma binafsi

Pamoja na kuwaelekeza washiriki kujifunza neno wakiwa peke yao, viongozi wa Kanisa wapange jinsi ya kulikutanisha Kanisa kwa kusudi la kuomba na kujifunza pamoja kwa namna ambayo si ya kawaida. (Ubunifu unaweza kufanyika kwa ushauri wa Mchungaji). Njia zifuatazo zaweza kutumika: Kuwagawa washiriki katika makundi madogo madogo na kuwa na daftari la kusimamia maendeleo yao Pia kuwe na semina za Unabii wa Danieli na Ufunuo Kanisani Simamia vizuri wajibu wa waalimu wa Shule ya Sabato Tafuta mbinu ya kuwahusisha washiriki wote katika program hizi za kulikoma za Kanisa na kulifundisha jinsi ya kufaya uinjilisti. Mwisho kabisa wapatie goli la uinjilisti kwa kila kikosi.

Kipimo

- Ongezeko la Idadi ya Washiriki wanaofanya uamsho na matengenezo huku wakikusudia kuwa kama Yesu katika tabia, huduma, na mtindo wao maisha pamoja na wale wanaowaongoza.
- Ongezeko la idadi ya Washiriki wanaotekeleza na kushirikishwa katika mzunguko wa program ya Makanisa yanayokua, katika kuwahudumia washiriki wenzao wa zamani, na washiriki wapya.
- Ongezeko la washiriki wanaoshirikishwa na kudhihirisha kuwa wamepata uzoefu katika zoezi la kuwalea washiriki wapya wanaoingia kanisani.
- Ongezeko la idadi ya washiriki waliorudi nyuma na wale ambao hawakufutwa ushirika katika suala zima la kuanza kuhudhuria tena ibada wazolikua wameanza kuziacha. (Kuona washiriki wakirejeshwa).

**KUWAFIKIA WENGINE** Tunao ujumbe wa uzima au mauti wa kuupatia ulimwengu (Tazama Ufunuo 14:6-12).

KUSUDI: Kumuongoza kila mshiriki kuhusika katika kuwahudumia wanadamu wengine wenye mahitaji, kushuhudia kweli za Biblia, na kuiongoza mioyo kumfuata Kristo na kujiunga na Kanisa la masalio.

### Jinsi ya Kuwafikia Wengine kupitia Idara ya Huduma binafsi

Moyo wa Utume wa Kanisa la Waadventista Wasabato, ni kuushuhudia ulimwengu huu ujumbe wa injili ya milele na kuwasogelea watu kwa karibu kwa njia ya kila mmoja wetu kuwafanya kazi ya injili kwa watu au mtu flani. Huduma binafsi kazi yake kubwa ni kutoa mafunzo, kutoa miongozo, na kuwaonesha watu umuhimu wa kila mshiriki kuhusika katika kazi hii ya mihimu sana. Kipengele hiki kitaelezewa zaidi ktk utekelezaji wa mpangokazi.

Kipimo

- Kuona ongezeko la idadi ya washiriki wanaobatizwa katika kanisa
- Kuona ongezeko la idadi ya washiriki wanaohusika katika huduma endelevu ya matendo ya huruma kwa jamii.
- Kuona ongezeko la idadi ya washiriki wanaohusikazoezi la ugawaji wa machapisho yaliyojaa kweli za mafundisho ya Biblia.
- Ongezeko la Idadi ya washiriki wanaohusika katika zoezi la kuendesha madarasa na mijadala ya Biblia iliyopangiliwa na yenye lengo maalum.
- Ongezeko la Idadi ya makanisa yanayofanya mikutano ya hadhara ya Injili ya neno la Mungu..

# Idara ya Huduma Binafsi

*Utekelezaji wa Mpangokazi*

MAKANISA YANAYOKUA

North East Tanzania Conference

**Makanisa Yanayokua**: TMI ni Mpangango wa kanisa la Ulimwengu

**Makanisa Yanayokua ni mpango gani hasa?** Mpango wa Makanisa yanayokua ni mkakati uliokusudiwa kutekeleza Mpangokazi wa Idara ya Huduma Binafsi. Ni mpango unaopalilia habari za Ushirikishwaji wa Kila Mshiriki (TMI) kwa kutoa mafunzo na miongozo, inayoelekeza katika utekelezaji wenye kutumi-ambinu zote za uinjilisti, kwa mtindo au mfano wa kilimo cha uongoaji wa roho uliofundishwa na Kristo mwenyewe

**Hizo nembo tano zinawakilisha nini?** Hizo nembo tano zinawakilisha mambo matano makubwa na ya muhimu katika uinjilisti wenye mafanikio.

- Moyo (Kama udongo) unaandaliwa kwa urafiki na huduma za kimahitaji.
- Mbegu za kweli ya neno la Mungu zinapaswa kupandwa kwa kutumia -- machapisho, vyombo vya habari, ushuhudiaji, na kuwaalika watu kujifunza Biblia kwa masomo yenye miongozo au kwa semina za neno la Mungu.
- Ni lazima tuipalilie nia ya mtu anayeonesha utayari wa kujifunza Biblia.
- Maamuzi ya kumfuata Kristo na Kulifuata neno lake ni mavuno ambayo tunapaswa kuyafanya kwa uinjilisti wa mtu mmoja mmoja au kwa hadhara.
- Mavuno hayo ni lazima yatunzwe kwa mpango maalum wa kuwafanya washiriki kuwa wanafunzi kwa namna endelevu.

**Makanisa Yanayokua ni mpango gani hasa?** Huu mpango wa makanisa yanayokua, kimsingi sio mpango wa North East Tanzania Conference bali ni mpango kwa kila Kanisa linalokusudia kukua katika ukomavu wa kiroho wa washiriki wake na ukomavu katika uinjilisti.

MAKANISA YANAYOKUA SANGU SDA CHURCH | MAKANISA YANAYOKUA SANGU SDA CHURCH | MAKANISA YANAYOKUA SANGU SDA CHURCH | MAKANISA YANAYOKUA SANGU SDA CHURCH | MAKANISA YANAYOKUA SANGU SDA CHURCH

Mpango Huu ni kwa ajili ya Kanisa Mahalia

## Umuhimu wa Mambo haya MATANO kwa Kanisa Linalokua

Mpango wa makanisa yanayokua, unayawezesha makanisa; si tu kumshirikisha kila mshiriki, bali pia kulifanya hilo kwa njia ambayo inalipelekea kanisa kukua. Kanisa linaweza kuwa na ushirikishwaji wa washiriki wote katika huduma, lakini kama hizo huduma zinahusisha aina moja tu ya huduma au mbili tu, itapelekea hali ya kiroho ya kanisa kuwa dhaifu na hatimaye kudumaa. Kiongozi azingatie haya yafuatayo:

- *Ikiwa kila muumini kanisani anashiriki kikamilifu katika kuuandaa udongo wa mioyo kama shamba, kwa kufanya huduma kwa jamii; na wakati uo huo watu wachache tu wakashiriki katika kufundisha neno la Mungu, mioyo mingi haitaguswa na neno la Mungu.*
- *Ikiwa tunafundisha Ukweli wa neno kwa majirani zetu, lakini kamwe tusifanye matendo ya huruma kwa jamii inayotuzunguka, ujumbe wetu utakosa wasikilizaji na ushuhudiaji wa neno utaharibika.*
- *Ikiwa tutagawa machapisho, lakini tufanye ufuatiliaji kwa mwendelezo wa mafundisho ya Biblia na kufanya wito wa kukatisha shauri, tutashindwa kufanya mavuno ya mioyo aliyoikomboa Yesu.*
- *Lakini pia ikiwa tutapata uzoefu wa kuvuna mioyo mingi sana, lakini tukashindwa kuwalea washiriki kwa mpango unaoeleweka na makini wa kuwafanya kuwa wanafunzi, itapelekea watu kurudi nyuma na kuasi baada ya muda mfupi sana.*

Makanisa ni lazima yawe na uinjilisti wenye uwiano sawia katika mpango wa uinjilisti, ambapo kila mshiriki anatambua na kuelewa umuhimu wa kila kipengele katika zoezi zima la uongoaji wa roho. Ni kwa njia hii peke yake (ya kuhusisha vipengele vyote) Ushirikishwaji wa Kila Mshiriki Kikamilifu, utapelekea Ukuaji wa Kila Kanisa Kikamilifu.

Sasa basi, goli la kila kipengele katika mpango wa Makanisa Yanayokua, linagusa lengo moja wapo katika hatua tano za kukua kwa Kanisa:

**HAKIKISHA KILA MTU ANASHIRIKI**

**01. Kila Mshiriki kwa Makanisa Yote Kushiriki katika Program za Huduma kwa Jamii**

**02. Huduma ya Uinjilisti wa Vitabu iliyo hai, kwa kila Kanisa na Kila Mshiriki**

**03. Program yenye nguvu, ya Mpango Maalum wa Kujifunza Biblia**

**04. Mpango wa Mikutano ya Hadhara ya mara kwa mara kwa kila Kanisa**

**05. Program ya Kuwafanya Washiriki kuwa wanafunzi wa kila Kanisa**

## MIONGOZO kwa Makanisa Kutimiza Mpango Huu


Kwa kila hatua ya mpangokazi huu wa Makanisa Yanayokua, Idara ya Shule ya Sabato na Huduma Binafsi zimeandaa na kutoka mwongozo wa kuyawezesha makanisa kufanikiwa katika ukuaji na shughuli nzima ya uinjilisti. Hapa kuna baadhi ya mambo ambayo washiriki wanapaswa kuelekezwa na kufundishwa jinsi yanavyofanyika. Kama yakifanywa vizuri kwa ushirikiano wa viongozi wa Idara mbalimbali, Wazee wa Makanisa na Mchungaji, matokeo yake yatakuwa makubwa na yenye kushangaza:

## ANDAA MAZINGIRA




- **Mwongozo kwa Huduma za Afya:** Ni wajibu wa viongozi wa Kanisa kukaa na kupanga kwa pamoja, jinsi makanisa yanavyoweza kutoa huduma za afya bure bila malipo kwa lengo la kufungua milango ya injili. Mfano: Mnaweza kuwa na Jim Club, Ushari na saha, n.k. Ubunifu uzingatiwe kilingana na mazingira; taaluma za watu zitumiwe ili kufanikisha
- **Mwongozo wa Hudma kwa Jamii:** Ni wajibu wa viongozi wa Kanisa, kulifundisha Kanisa, na kubuni mbinu za kufanya huduma kwa jamii. Hii inahusisha kuionesha jamii kuwa tunaipenda kwa kuifanyia jambo flani au mradi flani endelevu unaoashiria tunaijali jamii na kuipenda.

## PANDA MBEGU ZA INJILI




- **Huduma ya Ugawaji wa Machapisho:** Washiriki wafundishwe kwa vitendo jinsi ya kufanya program imara ya uinjilisti kwa njia ya machapisho na vyombo vya habari. Viongozi watengeneze bajeti, malengo, mapendekezo ya njia za utekelezaji na vipimo vya mafanikio.
- **Utume 365:** Wasisitize washiriki kushiriki katika kupanda mbegu za neno la Mungu, si kwa matukio bali kulifanya hili kuwa mtindo wao wa maisha wa kila siku kwa mwaka mzima. Wapendekezee kugawa chapisho au kitabu angalau kimoja kwa kila juma, kila mtu kulingana na uwezo wake.
- **Madarasa ya Biblia:** Waelekeze na uwafundishe kwa vitendo jinsi ya kuwaalika watu kujiunga na madarasa ya kujifunza Biblia ambayo ni yale yale uliyowagawa washiriki wako hapo mwanzoni katika program ya “KUWAFIKIA WENZETU.”

## PALILIA MBEGU ZINAZOKUA

- **Fufua/Anzisha Shule za Biblia:** Kila kanisa lianzishe kozi maalum za kujifunza mafundisho ya Biblia. Lakini pia kanisa linapaswa kukufua au kuanzisha kozi za mafundisho ya Unabii wa Biblia na mafundisho ya Imani za Msingi kwa namna inayovutia. Hakikisha watu wanaelewa, usikimbilie kumaliza au kuonyesha unajua sana.
- **Miongozo ya Neno:** Kiongozi anapaswa kuandaa miongozo ya kujifunza mafundisho makuu. Kiongozi ashirikiane na kamati ya huduma ili kuweka mpango na kubuni mbinu ya kuwavuta watu kuja kujifunza Biblia, na kuwapatia notsi za mafundisho wahudhuriaji.




  Kiongozi wa huduma amuone Mchungaji wake ili apate mashauri ya namna ya kupata miongozo ya kujifunza Biblia inayoendana na mazingira waliyonayo na kiwango cha wastani wa uelewa wa neno kwa washiriki waliopo Kanisani na wanafunzi wapya wa Biblia.

## WEKA MKAKATI WA MAVUNO

- **Miongozo ya Mahubiri ya hadhara:** Kwa sehemu kubwa kanisa limekuwa likifanya uinjilisti huu wa mahubiri ya hadhara kama njia kuu ya uinjilisti. Tumetegemea sana wainjilisti flani na wahubiri maarufu na ndivyo tumefanya kwa muda mrefu. Sasa ni muda wa kurejea miongozo ya namna uinjilisti huu unavyopaswa kufanywa. Katika kila darasa, au kila fundisho, watu waelekezwe kwa upole kukata shauri kila baada ya muda hatua flani ya uelewa. Wafundishe washiriki jinsi ya kukatisha shauri kwa vitendo.





- **Kuwaandaa Washiriki Kabla ya Ubatizo**

  Kila mtu anayebatizwa, ikiwa anaweza kusoma, apewe Mafundisho ya Imani za Msingi mkononi, kabla ya kubatizwa na baada ya ubatizo ianzishwe kozi maalum na makini kwa kila mtu anayebatizwa. Mzee wa Kanisa anayehusika na Kamati ya malezi ya Waumini Kanisani, ahakikishe hili jambo lina-mkakati maalum, makini na uliopangiliwa vizuri.

  Mtu anapobatizwa sikabidhiwe kwa mtu mmoja tu. Akabidhiwe kwa Kikosi cha Shule ya Sabato, ili kimlee. Utafiti unaonesha wale wasiopata marafiki 6 - 8 wanapobatizwa, hurudi nyuma na kuiacha imani.

# WEKA MKAKATI WA MAVUNO





- **Mwongozo wa Kufanya Wanafunzi:** Idara ya Huduma inapaswa kuwa na  mpango wa program maalum ya kuwahifadhi washiriki waliobatizwa tayari kwa kuhakikisha wanafundishwa jinsi ya kujifunza Biblia wakiwa wenyewe na kuwagawanya ktk vikosi vidogo vidogo vya utendaji. Pia Shule ya Sabato ihakikishe inayafuatilia kwa ukaribu vikosi vyote vya utendaji hasa vile vilivyokabidhiwa kuwalea washiriki wapya. Kamati ya Shule ya Sabatoinapaswa kukaa mara kwa mara kutathmini maendeleo ya shule ya Sabato na maendeleo ya washiriki wake wapya. Pia kamati ya malezi ihakikishe inafanya tathmini ya malezi ya washiriki hao wapya.

  Kumfanya mtu kuwa mwanafunzi inagusa Ibada Binafsi, Ushuhudiaji, Kushiriki ktk Program za Kanisa, Mtindo wa Maisha ya Kikristo pamoja na Program ya Uinjilisti kama mtindo wake wa maisha ya Kikristo. Hwa washiriki wapya waingizwe ktk hili mzunguko huu kila wanapobatizwa.

## KUZA Program Maalum ya Maombi

Mikakati iliyowekwa kwa ustadi mzuri na utaalam haitapelekea Kanisa Kukua ikiwa Haijabarikiwa na Roho wa Mungu. Katika kila hatua ya Program  ya Makanisa yanayokua, tunapaswa kuwa na mahusiano mazuri na Mungu wetu kwa njia ya maombi ya dhati. Tunaweza kupanda, tunaweza kupalilia, lakini Mungu pekee ndiye anayeweza kuleta Ukuaji. (1 Wakorintho 3:6). Mpangokazi wa Idara ya Huduma Binafsi inayatia moyo makanisa kufanya uinjilisti wenye tija lakini ni lazima na muhimu tuwe na mahusianon na Mungu maana pasipo uwepo wa Mungu hatuwezi kuwa na mafanikio katika kazi.

“Ni lazima tuifanyie kazi mioyo kwa maombi mengi, maana ni kwa njia hii pekee tunaweza kuifikia mioyo. Hii si kazi yako, lakini ni kazi ya Kristo ambaye yuko upande wako, na Yeye ndiye anayeigusa mioyo”
(Evangelism, uk. 341)




Unaweza kufanya Ubunifu wa Kuwa na Kadi za Maombi ambazo zinawakumbusha kuombea kila hatua ya uinjilisti tunayoifanya.

## Tafakari nadharia hizi za Mtindo wa Uinjilisti

Mtindo wa Njia Moja vs. Mtindo wa Makanisa Yanayokua

Mtindo wa Makanisa yanayokua unahusika na uinjilisti katika mapana yake na unagusa aina zote za uinjilisti, tofauti na mtindo wa kutegemea njia moja tu. Mtindo wa kutegemea njia moja peke yake hupelekea kushindwa kuona umuhimu wa vipengele vingine muhimu katika program ya uongoaji wa roho. Inapelekea pia kuziona mbinu nyingine za uinjilisti katika hali ya ushindani badalaya kuziona kama ngazi za uinjilisti wenye mafanikio.

- Njia Moja Pekee: "Kanisa langu linafanya unjilisti mara moja kwa mwaka"

  **Njia Zote za Uinjilisti:** Katika njia hii, mikutano ya injili haipaswi kufanyika mara moja au mara mbili tu kwa mwaka; na kanisa likaridhika kuwa tumefanya uinjilisti. Uinjilisti wenye mafanikio, unafanyika kila wakati kwa kuzingatia vipengele vya matendo ya huruma, kufundisha neno na kuwalea wale wanaomkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao binafsi.

- Njia Moja Pekee: "Kuwapatia watu mahitaji yao ya kimwili na kihisia ndio uinjilisti halisi."

  **Njia Zote za Uinjilisti:** Kugusa mahitaji ya watu ni jambo la muhimu sana katika uinjilisti, lakini sio jambo pekee la muhimu. Umuhimu wa kugusa mahitaji ya watu hauwezi kamwe kuondoa umuhimu wa kuwafundisha ukweli wa neno la Mungu.



- Njia Moja Pekee: "Kukazania kufanya uinjilisti wa nje ni kusahau kuwalea na kuwatunza wale tulionao kanisani."

  **Njia Zote za Uinjilisti:** Kulea ni hali ya kumjali na kumtunza mtu kwa namna inayomfanya akue kiroho -- lakini kwa upande mwingine kuwahusisha sana washiriki katika uinjilisti ni jambo la muhimu ili kuwafanya washiriki wakue kiroho! "Hebu wachungaji na wawafunsishe washiriki kwamba ili kukua kiroho, wanapaswa kubeba mzigo wa ambao Bwana amewatwika juu yao - mzigo wa kuiongoza mioyo katika ukweli." (Christian Service, p. 69).

▶ Njia Moja Pekee: "Mimi uinjilisti wangu ni Uinjilisti kwa njia ya Urafiki."

**Njia Zote za Uinjilisti:** Ni jambo jema kabisa kufanya uinjilisti wa kiurafiki! Bali pia imetupasa kukumbuka kuwa hakuna mkulima anayeandaa shamba kisha asipande mbegu wala kwenda kuvuna. Bwana wetu ametupatia upendeleo wa pekee wa kuwaongoza rafiki zetu katika ile kweli! Wito kwa mioyo yote iliyosamehewa, yaani wale waifurahiayo nuru, kuufanya ukweli ujulikane kwa wengine." Christian Service, p. 37)



▶ Njia Moja Pekee: "__________________ndio uinjilisti wa kweli."

Idara ya Mawasiliano ingaliweza kusema "Teknolojia ndiyo njia pekee inayofaa." Lakini pia ADRA wangeweza kusema "Sisi ndio kila kitu." Wakati huo huo Idara ya Uchapishaji ingeweza kusema "Sisi ndio pekee tunaofanya uinjilisti wa kweli." Bado Idara ya Afya na Wanawake, n.k.

**Njia Zote za Uinjilisti:** Katika Kanisa lilonakua, kila idara ndani ya Kanisa ni ya muhimu sana katika uinjilisti na katika kukamilisha Utume wa Kanisa. Lakini pamoja na umuhimu huo kila idara inapaswa kupanga uinjilisti kwa kushirikiana na Idara nyingine katika kuiongoza mioyo kwenye ukweli wa neno la Mungu. Kila Idara ikisema ijitegemee, HAKUTAKUA NA MAFANANIO

▶ Njia Moja Pekee: "Uinjilisti wa Mtu mmoja mmoja ni wa muhimu sana kuliko uinjilisti wa mahubiri ya hadhara." Au, mialiko ya kumtembelea mtu nyumbani ni bora zaidi kuliko kuwasiliana naye tandaoni." Sasa basi tuache mitandao ili tufanye ya uso kwa uso."

**Njia Zote za Uinjilisti:** Katika makanisa yanayokua, njia zote za uinjilisti zinatumika. Isaya 32:20 anasema "Heri ninyi mpandao mbegu kando ya maji yote..." Nabii naye anasema "Njia zote zinapounganishwa (Mikutano ya Hadhara na uinjilisti wa mtu mmoja mmoja}, pamoja na baraka za Mungu, matokeo yake, yatakua kazi iliyo kamilifu na bora."

Tusiyaache makanisa yetu kubaki na njia moja peke yake inayotumika katika kutimiza utume. Tafadhali tuone nama njema ya kuziunganisha Idara zote na kupanga jinsi kila Idara kanisani itakavyoshiriki katika hatua flani ya utekelezaji wa mpango wa uinjilisti kwa njia ya makanisa yanayokua.

► Njia Moja Pekee: “Idadi kubwa ya wabatizwa ni ushahidi wa mafanikio katika uinjilisti.”

**Njia Zote za Uinjilisti:** ”Sio lazima ubatizo uwe ishara ya mafanikio ya kazi waliyofanya washiriki kanisani. Ikiwa tutabatiza haraka haraka sana bila kuwa na muda wa kuyaandaa mavuno, inaweza kusababisha changamoto zingine baadae, ambazo wengi wetu huwa hawazioni mapema. “Uangalifu mkubwa unapaswa kufanyika katika kuwakubali watu kuwa washiriki katika Kanisa; kwani Shetani anazo mbinu danganyifu ambazo hutumika kwa makusudi ya kuwaingiza ndugu wasio wa kweli katika Kanisa, na kupitia hao anaweza kufanya kazi yake kwa mafanikio ili kudhoofisha kazi ya Mungu.” (Evangelism, uk. 131).

► Njia Moja Pekee: “Ubatizo ndilo lengo kuu la uinjilisti ”

**Njia Zote za Uinjilisti:** Ni kweli kabisa kwamba Ubatizo ni goli (Tazama Mathayo 28:19), lakini bado sio goli pekee, katika program za uongoaji wa roho. Ni lazima tuwakomaze na kuwafundisha washiriki wapya ili tuwe na wanafunzi waliosimikwa vizuri na wanaoweza kutengeneza wanafunzi wengine. ”Roho moja iliyoongoka kupitia ukweli, itakua ya muhimu sana katika kuziongoa roho nyingine, na hapo patakuwa na ongezeko la kila wakati katika baraka na wanaookolewa. (Christian Service, uk. 121).

TMI

MAKANISA YANAYOKUA

[North East Tanzania Conference]

Sabbath School and Personal Ministries

General Conference Sabbath School and Personal Ministries Department
12501 Old Columbia Pike | Silver Spring, MD 20904 | 301-680-6182